G6

MTAALA WA UMILISI

KISWAHILI

Mwongozo wa kusahisha

1. **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.(alama 4)**

Rununu yake ilikiriza mara kadhaa lakini akashindwa kuiwahi. Kichwa chake kilimwanga vilivyo. Usiku uliotangulia alikuwa amepiga maji na kulewa chakari. Hakuelewa alivyofika kitandani pake. Mlaraha alikuwa mwizi hatari. Hii ilikuwa shughuli haramu na hatari kweli kweli. Aliitazama simu yake ya mkononi ilivyokuwa imechakaa. Ghafla, mlango wake ukabishwa kwa kishindo. Alisita kidogo huku akijiuliza kama kweli alikuwa na ahadi ya kukutana na yeyote asubuhi hiyo.

Kufumba na kufumbua, pu! Mlango ulipigwa teke na kuanguka kando. Mlangoni walisimama maafisa wanne wa polisi na bastola huku wawili wakiwa na pingu mikononi. Mlaraha aliinua mikono juu ishara ya kusalimu amri. Moyoni alijua kuwa zake arubaini zilikuwa zimetimia. Naam, uhalifu haulipi chochote.

a. Mlaraha hakuweza kuiwahi rununu yake kwa kuwa **kichwa chake kilikuwa kizito.**
b. Chagua orodha ya sifa za Mlaraha kulingana na kifungu. **Mlevi, mwizi.**
c. Ni kweli kuwa waliobisha mlango walikuwa. **maafisa wa polisi.**
d. Methali gani inayoweza kutumika kufupishia kisa hiki? **Siku za mwizi ni arubaini.**

2. **Sema kifungu kifuatacho kisha ulibu maswali. (alama 3)**

Uhalifu ni hali ya kutenda kinyume na zinavyohitaji sheria za nchi ambazo siku zote huongozwa na katiba. Kunavyo viwango mbalimbali vya uhalifu katika jamii. Uhalifu hutendeka katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, kuna njia kadhaa za kukabiliana na uhalifu. Kwanza, wananchi wakiacha tabia za kuwaficha wahalifu miongoni mwao, uhalifu utapungua. Vile vile, wale ambao hupokea hongo wanastahili kufunguliwa mashtaka. Si hayo tu, uhalifu aidha huweza kupungua iwapo sehemu mbalimbali za umma kama vile afisini zitawekewa kamera za siri. Kwa jumla, kila mwanajamii akisimama kidete kupambana na uhalifu, tutaweza kujivunia kupungua kwa uhalifu.

a. Mwandishi ametaja njia ngapi za kukabiliana na uhalifu?**Tatu.**
b. Kulingana na habari hii, kamera za siri zinaweza kudhibiti uhalifu.**afisini.**
c. Kwa jumla, jukumu la kudhibiti uhalifu ni jukumu la nani? **Kila mmoja.**

3. **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.(alama 3)**

Shughuli kama vile kuogelea, kandanda, riadha na urukaji viunzi huitwa michezo. Shughuli hizi si muhimu tu katika kuijenga miili yetu bali pia huchangia kuwaleta watu pamoja. Michezo baina ya shule mbalimbali huwaleta wanafunzi pamoja ambapo wao huweza kubadilishana mawazo yanayoweza kuinua viwango vyao vya kimasomo.